OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA
MTWARA

Namba za simu
Mkuu wa shule: **0652838425,**
Makamu mkuu wa shule: **0656095634**
Namba ya patroni: **0783018679**

Shule ya sekondari Mnyambe,
S. L. P 339,
Newala.

Mzazi / mlezi wa mwanafunzi .....
.....
S. L. P .....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MNYAMBE 2021/ 2022

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **2021 / 2022** katika Shule ya sekondari Mnyambe. Shule ipo umbali wa KM 35 kutoka Newala mjini. Gharama ya usafiri kutoka hapo hadi shuleni ni kati ya **4000/=** na **5000/=** inategemea na wakati. Kumbuka shule haitawajibika kukulipia gharama hizo.
Muhula wa masomo utaanza tarehe **05/07/2021** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **03/07/2021**
Baada ya pongezi hizo napenda kukujulisha mahitaji ya shule hii.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 (a) **Sare ya shule**

i) Suruwali mbili (2) dark blue (Tumia kitambaa grade 1) zenye upana nchi 7.5 chini, mifuko mitatu, **Aje nazo**
ii) Mashati mawili (2) meupe tetroni ya mikono mirefu, aje nayo
iii) . Tai mbili (2) ndefu rangi hiyo ya suruali, **Aje nazo.** Sweta mbili (2) za dark blue zinapatikana shuleni kwa Tsh. **15,000/= k**wa kila moja.
iv) Viatu jozi mbili rangi nyeusi vyenye visigino vifupi.
v) Soksi nyeusi jozi mbili.
vi) T-shirt light blue mbili zinapatikana shuleni kwa Tsh. **15,000/=** kwa kila moja
vii) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
viii) Surualia mbili nyeusi za kushindia (shamba dress) **aje nazo**, upana nchi (7.5) na mifuko mitatu.

NB: Fedha za sare ya shule ziingizwe kwenye account namba 70806600382 NMB – mnyambe sekondary school project account (kumbuka kuja na pay in slip, pesa tasilimu hazitapokelewa)

2.1 (b) **Sare za michezo**

i. Traki suti moja blue
ii. Bukta mbili blue
iii. Fulana mbili blue zisizo na maandishi(jezi)
iv. Stocking soksi rangi ya blue
v. Raba jozi moja

(Sare zote hizo za michezo anapaswa kuja nazo)

2.2: Ada na michango

a) Ada ya shule ni Tsh. **70,000/=** (elfu sabini tu) kwa mwaka. Pesa hiyo unaweza kulipa yote au kwa awamu mbili Tsh. **35,000/=** kwa kila muhula. Pesa hizo zilip we katika **A/C NO. 70801200049 NMB MNYAMBE SEKONDARI (tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)**

b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi

i. Ukarabati samani Tsh. **15,000/=** kwa mwaka.
ii. Kitambulisho na picha Tsh. **6,000/=**
iii. Taaluma Tsh. **20,000/=** kwa mwaka
iv. Wapishi walinzi na vibarua Tsh. **30,000/=** kwa mwaka.
v. Huduma ya kwanza Tsh. **20,000/=**
vi. Kukodi godolo kwa muhula Tsh.**10,000/=**
vii. Tahadhali ni Tsh. **5,000/=** haitarejeshwa
viii. Mock **Tsh.20,000/=**

NB: Fedha hizo ziingizwe kwenye account namba 70806600382 NMB – mnyambe sekondary school project account (kumbuka kuja na pay in slip, pesa tasilimu hazitapokelewa)

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

i. Result slip (kivuli) ya kidato cha nne.
ii. File / jalada la kutunzia mitihani
iii. Dawa ya chooni lita 5
iv. Scientific calculator
v. Vitabu vya masomo husika
vi. Daftari kubwa (counter book quire 4) 10
vii. Rimu A4 1 na graph paper kitabu 1 kwa mwaka
viii. Ndoo za maji 2 za lita 10 zenye mifuniko
ix. Vyombo vya chakula (sahani, kijiko, kikombe na bakuli)
x. Jembe 1, Fyekeo 1, Reki 1, Fagio ya ndani 1, panga 1,
xi. Shuka mbili rangi ya pink, blanketi 1, mto 1, foronya ya rangi ya pink 1, taulo 1 na chandarua
xii. Dissecting kit 1 kwa wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanfunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kufuga ndevu
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uwasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa.
x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yanayovunja sheria ya nchi
xi. Kumiliki, kukutwa au kutumia laini / simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xii. Kudharau bendera ya taifa
xiii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xiv. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xv. Kutembelea majumba au sehemu za starehe na nyumba za kulala wageni
xvi. Uharibifu wa mali ya shule kwa makusudi

4. VIAMBATANISHO NA FOMU MAALUMU

Uje na taarifa zifuatazo zikiwa zimekamilika

i Kivuli cha cheti cha kuzaliwa (Birth certificate)
ii Taarifa binafsi kuhusu mwanafunzi
iii Mkataba wa kutoshiriki migomo , vurugu ama makosa ya jinai.
iv Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination certificate) kilichotthibitishwa na daktari.
v Fomu ya mzazi / mlezi kukiri, kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

A. Shule yetu inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na Elimu hapa Tanzania. Kwa hiyo mwanafunzi anatakiwa azingatie mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa baada ya kuripoti shuleni.
B. Awe na heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, walimu na wanafunzi kwa ujumla.
C. Ni lazima awe na mahudhurio mazuri katika kazi zote za shule
D. Ni muhimu kuwahi katika kila shughuli na kazi zingine utakazopewa.
E. Ni vema kuifahamu mipaka ya shule na kuheshimu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo.
F. Kutunza usafi binafsi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
G. Kuvaa sare sahihi ya shule na kwa usahihi wakati wote inapotakiwa.

H. Ni lazima uweke mkazo katika masomo,usome kwa bidii na jitihada zako zionekane kwa walimu na wazazi wako.

I. Mzazi unashauriwa kuja shuleni kumsalimiia mtoto wako kila jumamosi ya mwisho wa mwezi kwa pale inapohitajika.

(***tafadhari soma kwa makini maagizo / maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu)***

karibu katika shule yetu

.....

ISSA M. MKUTI

MKUU WA SHULE

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

THE PRESIDENT'S OFFICE REGINAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

Mnyambe Secondary school,

P. O. Box 339,

Medical Officer, Newala.

……

STUDET'S FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by Medical Officer in respect of all students joining in our school.

Student's full name……

Age …… Year ……

Sex ……

Blood count (red and White) ……

Urine ……

Stool ……

Venereal Disease ……

T. B ……

Ears ……

Eyes ……

Spleen ……

Chest ……

ADITIONAL INFORMATION

If any, Eg; Physical defects

Arm or leg impairments, chronic or family diseases

Etc

……

……

I certify that she / he is fit / unfit to pursue education as stated.

Signature …… Station ……

Designation …… Date ……

TAARIFA BINAFSI KWA MWANAFUNZI

SEHEMU A

Jina kamili (kwa herufi kubwa) ……
Tarehe ya kuzaliwa ……
Jina la baba / mama / mlezi ……
Kazi yake …… Namba ya simu ……
Anuani ya nyumbani……Barua pepe ……
Kijiji ……Kata …… Tarafa ……..
Wilaya …… Mkoa ……
Kabila …… Dini ……
Dhehebu …… Uraia ……
Mambo unayopendele kufanya nje ya masomo (kwa mfano: michezo, Bustani na kuchora)
1……2……3……4……

SEHEMU C

ADA ITALIPWA NA ……

SEHEMU D

Ninaahidi kuwa na tabia nzuri na mwenye bidii katika masomo yangu. Nimesoma maelezo yote na kuzielewa sheria za shule, Mungu nisaidie.
Sahihi ya mwanafunzi …… Sahihi ya mzazi / mlezi…….
Tarehe …… Tarehe …… 7

FOMU YA MAKUBALIANO NA MZAZI / MLEZI

Mimi …….ambae ni mzazi / mlezi wa …….

(nakubali au sikubali masharti yafuatayo) kata neno mja

(a) Nafasi aliyopewa kijana wangu kujiunga na kidato cha tano katika mwaka wa masomo …….

(b) Kijana wangu kufuata sheria, maagizo na masharti yote ya shule ya sekondari Mnyambe.

(c) Kulipa Ada na michango yote itakayoelekezwa na shule.

(d) Kumpatia mwanangu mahitajii yote ya shule kama ualivyoorodheshwa na shule.

(e) Kufuatilia kwa karibu maendeleo ya kila siku ya mwanangu tabia, mwenendo na taaluma

(f) Kupokea taarifa zote kutoka shuleni zinazomuhusu mwanangu na kuzifanyia kazi kwa wakati.

Asante

JINA……SAHIHI……TAREHE…….

MKATABA WA KUTOJIHUSISHA NA VURUGU, MGOMO FUJO NA MAKOSA YA JINAI

(Fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni)

Mimi .....ambae ni mwanafunzi

wa kidato cha .....katika shule hii naahidi kutojihusisha kwa namna yoyote katika migomo, fujo au kosa lolote la jinai ambalo litahatalisha amani au litakalokuwa kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za shule.

Endapo ikithibitika kuwa nimetenda kosa au makosa tajwa hapo juu sitakuwa na pingamizi juu ya hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa dhidi yangu

Jina la mwanfunzi .....

Sahihi ya mwanafunzi .....

Tarehe .....

Jina la mzazi / mlezi .....

Sahihi ya mzazi / mlezi .....

Tarehe .....